# Usalama wa Abiria Mtoto

Fuata hatua hizi ili kusaidia kuhakikishia kuwa watoto wako wapo salama garini.

**WATOTO WALIO CHINI YA UMRI WA MIAKA 13 SHARTI WAKETI KWENYE KITI CHA NYUMA.**



## KITI CHA WATOTO KINACHOTAZAMA UPANDE WA NYUMA WA GARI

- Watoto walio chini ya umri wa miaka 2 sharti wakalie kiti cha watoto kinachotazama upande wa nyuma wa gari.
- Kamwe usiweke kiti cha watoto kinachotazama upande wa nyuma wa gari, mbele ya mfuko wa hewa unaoweza kulipuka.
- Usitumie kiti cha gari kama sehemu ya kulala nje ya gari.




## KITI CHA WATOTO KINACHOTAZAMA UPANDE WA MBELE WA GARI

- Watoto walio chini ya umri wa miaka 5 sharti wakalie kiti cha watoto kinachotazama upande wa mbele wa gari kilichofungwa vizuri wanaposafiri.
- Kila mara tumia teta yenye kiti cha watoto kinachotazama upande wa mbele wa gari - soma mwongozo wa kiti cha watoto na gari lako ili kujua zaidi.



## KITI CHA WATOTO CHA KUWAONGEZEA KIMO

- Watoto ambao hawaketi kwenye kiti cha gari cha watoto sharti watumie kiti cha watoto cha kuwaongezea kimo ili wafikie kimo cha kufunga mkanda wa usalama ifaavyo hadi wafikie umri wa miaka 8.
- Watoto wengi wanahitaji kiti cha watoto cha kuwaongezea kimo wanapokuwa na zaidi ya umri wa miaka 8 kwa ajili ya usalama wao.



## MKANDA WA USALAMA

- Watoto walio chini ya umri wa miaka 18 ambao hawatumii kiti cha gari kilichofungwa kwa uthabiti wanaposafiri au kiti cha watoto cha kuwaongezea kimo sharti wawe wamefunga mkanda wa usalama.
- Hakikisha kuwa kila mtu kwenye gari lako anatumia mkanda wa usalama kwa kila safari.

**MPANGO WA USALAMA WA ABIRIA MTOTO**

**802-847-1215 AU 802-847-9988 (Huduma za Ukalimani)**

THE University of Vermont Children's Hospital